PREVENT • FIGHT • EDUCATE
PCCB
ERADICATE CORRUPTION

JARIDA

LA TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

ISSN:0856 - 7670 TOLEO MAALUMU JULAI 2023

RAIS SAMIA:
AFRIKA SI SALAMA KWA WALARUSHWA

www.pccb.go.tz

Ukiwa na maoni au taarifa ya vitendo vya rushwa ,wasiliana nasi kupitia Namba zifuatazo
MKURUGENZI MKUU,
Mtaa wa Jamhuri S.L.P.1291, 41101 Dodoma,Tanzania.
Simu: (026)2323316, Nukushi: (026) 2323332,
Baruapepe: dgeneral@pccb.go.tz | Wavuti:www.pccb.go.tz

Barabara ya Moshi Nairobi, S.L.P. 1055
Simu: +255 27 250 3538 / 250 7928
Nukushi +255 27 250 5973
Baruapepe: rbcarusha@pccb.go.tz
23103 ARUSHA

Mtaa wa Kilimani, S.L.P. 1175
Simu: +255 26 232 2003 / 232 2695
Nukushi: +255 26 232 0003
Baruapepe: rbcdodoma@pccb.go.tz
41101 DODOMA

Mtaa wa Nyanza, S.L.P. 38
Simu: +255 28 252 0004
Nukushi: +255 28 252 0004
Baruapepe: rbcgeita@pccb.go.tz
30101 GEITA

Mtaa wa 16 Urambo, S.L.P. 6420
Simu: +255 22 213 2954
Nukushi: +255 22 215 0047
Baruapepe: rbcilala@pccb.go.tz
11104 ILALA

Mtaa wa Gangilonga, S.L.P. 1575
Simu: +255 26 270 0156
Nukushi: +255 26 270 3014
Baruapepe: rbciringa@pccb.go.tz
51108 IRINGA

Mtaa wa Pwani Karume, S.L.P. 1138
Simu: +255 28 222 084 / 222 0491
Nukushi: +255 28 222 0534
Baruapepe: rbckagera@pccb.go.tz
35111 KAGERA

Mtaa wa Kawajense, S.L.P. 275
Simu: +255 25 282 0613
Nukushi: +255 25 282 0613
Baruapepe: rbckatavi@pccb.go.tz
50101 KATAVI

Mtaa wa Metrological, S.L.P. 880
Simu: +255 28 280 2889
Nukushi: +255 28 280 4928
Baruapepe: rbckigoma@pccb.go.tz 47115
KIGOMA

Barabara ya Mashina, S.L.P. 1951
Simu: +255 27 275 0885
Nukushi: +255 27 275 0889
Baruapepe: rbckilimanjaro@pccb.go.tz
25102 KILIMANJARO

Mtaa wa Usalama Magomeni S.L.P. 90397
Simu: +255 652 409 165
Nukushi: +255 764 383 959
Baruapepe: rbckinondoni@pccb.go.tz
14101 KINONDONI

Mtaa wa Sheikhbad, S.L.P. 1004
Simu: +255 23 220 2456 / 222 799
Nukushi: +255 23 222 02215
Baruapepe: rbclindi@pccb.go.tz
65101 LINDI

Mtaa wa Bagala Miomboni, S.L.P. 386
Simu: +255 27 253 0255 / 6 / 70
Nukushi: +255 27 253 0448
Baruapepe: rbcmanyara@pccb.go.tz
27103 MANYARA

Mtaa wa Nyerere, S.L.P. 377
Simu: +255 28 262 3030
Nukushi: +255 28 262 3029
Baruapepe: rbcmara@pccb.go.tz
31109 MARA

Mtaa wa Mahakama Avenue, S.L.P.1419
Simu: +255 25 250 3566
Nukushi: +255 25 250 2859
Baruapepe: rbcmbeya@pccb.go.tz
53103 MBEYA

Mtaa wa King'ola, S.L.P. 845
Simu: +255 23 22 614 302
Nukushi: +255 23 22 614 478
Baruapepe: rbcmorogoro@pccb.go.tz
67109 MOROGORO

Mtaa wa Aga khan, S.L.P. 213
Simu: +255 23 233 4013
Nukushi: +255 23 233 3726
Baruapepe: rbcmtwara@pccb.go.tz
63104 MTWARA

Mtaa wa Posta, S.L.P. 2599
Simu: +255 28 250 0600
Nukushi: +255 28 250 0602
Baruapepe: rbcmwanza@pccb.go.tz
33101 MWANZA

Mtaa wa Kwivaa, S.L.P. 629
Simu: +255 26 278 2777
Nukushi: +255 26 278 2777
Baruapepe: rbcnjombe@pccb.go.tz
59101 NJOMBE

Mtaa wa Taasisi, S.L.P. 30261
Simu: +255 23 240 2658 / 240 2284 Nukushi: +255 23 240 2657
Baruapepe: rbcpwani@pccb.go.tz
61101 PWANI

Mtaa wa Mkoani, S.L.P. 273
Simu: +255 25 280 2426 / 280 2926
Nukushi: +255 25 280 0312
Baruapepe: rbcrukwa@pccb.go.tz
55103 RUKWA

Mtaa wa Mahenge, S.L.P. 926
Simu: +255 25 260 0613
Nukushi: +255 25 260 0663
Baruapepe: rbcruvuma@pccb.go.tz
57101 RUVUMA

Mtaa wa Uzunguni, S.L.P. 37
Simu: +255 28 276 2630
Nukushi: +255 28 276 3358
Baruapepe: rbcshinyanga@pccb.go.tz
37101 SHINYANGA

Mtaa wa Viwandani, S.L.P. 306
Simu: +255 28 270 0371
Nukushi: +255 28 270 0532
Baruapepe: rbcsimiyu@pccb.go.tz
39101 SIMIYU

Mtaa wa Boma, S.L.P. 484
Simu: +255 26 250 2305 / 2502550
Nukushi: +255 26 250 2550
Baruapepe: rbcsingida@pccb.go.tz
43108 SINGIDA

Mtaa wa Mwenge, S.L.P. 588
Simu: +255 25 258 0226
Nukushi: +255 25 258 0226
Baruapepe: rbcsongwe@pccb.go.tz
54201 SONGWE

Mtaa wa Kilimatinde, S.L.P. 1020
Simu: +255 26 260 4030 / 260 4311
Nukushi: +255 26 260 4039
Baruapepe: rbctabora@pccb.go.tz
45112 TABORA

Barabara ya Bombo Hospitali, S.L.P. 1953
Simu: +255 27 264 5186
Nukushi: +255 27 264 7885
Baruapepe: rbctanga@pccb.go.tz
21105 TANGA

Mtaa wa Uwanja wa Taifa, S.L.P. 42325
Simu: +255 22 285 0633
Nukushi: +255 22 285 0635
Baruapepe: rbctemeke@pccb.go.tz
15103 TEMEKE

Yaliyomo

1. TAHARIRI UK.3

2. RAIS SAMIA: AFRIKA SI SALAMA KWA WALARUSHWA UK.4

3. WADAU AFRIKA WASHIRIKI MATEMBEZI YA KUPINGA RUSHWA.....UK.6

4. MHE: JOAQUIM: MAPAMBANO DHIDI YA RUSHWA YATAUNDA AFRIKA TUITAKAYO.....UK.8

5. NI HESHIMA KWA TANZANIA KUWA MWENYEJI WA MAADHIMISHO YA SIKU YA MAPAMBANO DHIDI YA RUSHWA BARANI AFRIKA 2023.....UK.10

6. CP. HAMDUNI: TUMETUMIA MAADHIMISHO KUELIMISHA UMMA KUHUSU MAPAMBANO DHIDI YA RUSHWA UK.12

7. VIJANA WASHIRIKISHWE KATIKA MAPAMBANO DHIDI YA RUSHWA.....UK.14

8. WADAU WAPONGEZWA KWA JUHUDI ZAO KATIKA MAPAMBANO DHIDI YA RUSHWA UK.16

9. RAIS SAMIA: MAPAMBANO DHIDI YA RUSHWA YAMEOKOA ZAIDI YA SHILINGI BILIONI 139 .....UK.18

10. ZAECA: TUNASHIRIKIANA NA WADAU KUZUIA RUSHWA UK.19

Mhariri Mkuu
Matai Kirumbi

Wahariri Wasaidizi
Miriam Chisoro
Sarah Chodota

Waandishi
Eldora Liwa
Miriam Chisoro
Sarah Chodota
Tezra Nkonya
Casiani Magogo

Wapiga Picha
Kenneth Ntandu
Amina Haroun Khamis

Msanifu
Faisal Balekao

Tahariri

Inawezakana kuifanya Afrika mahali pasipokuwa salama kwa walarushwa

Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alikuwa mgeni rasmi katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika yaliyofanyika jijini Arusha, Tanzania Julai 11, 2023. Maadhimisho hayo ya mwaka huu yaliambatana na maadhimisho ya miaka 20 ya utekelezaji wa Mkataba wa Umoja wa Afrika wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa wa mwaka 2003.

Akihutubia mamia ya washiriki wa maadhimisho hayo Mhe. Rais Samia alitahadharisha kuwa Afrika si salama kwa walarushwa na kwamba bara hili si kichaka cha kuficha fedha zilizotokana na rushwa au kufuga wala rushwa. "*Tunataka dunia nzima ifahamu kuwa, Afrika si salama kwa walarushwa na hilo lionekane kwa kupitia vitendo vyetu dhidi ya rushwa*", alibainisha Rais Samia.

Sisi tunamuunga mkono Rais Samia kuwa Afrika si salama kwa walarushwa. Pia, tunaunga mkono maelekezo yake kuwa ni matendo yetu Waafrika, wewe na mimi, yanayopaswa kuudhihirishia ulimwengu kuwa nchi zetu za bara la Afrika si salama kwa walarushwa, si vichaka vya kufuga walarushwa wala vya kufichia fedha zilizotokana na vitendo vya rushwa.

Maadhimisho ya mwaka huu ya Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika yamefanyika kwa mara ya kwanza kibara nchini Tanzania; si nchi zote zilizosaini na kuridhia Mkataba wa Umoja wa Afrika wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa zilishiriki. Nchi zilizoshiriki zilikuwa Ivory Coast, Zimbabwe, Zambia, Cameroon, Burundi, Liberia, Djibouti, Afrika Kusini, Uganda, Congo Brazaville, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC) na Mauritius.

Nyingine ni Sudani Kusini, Rwanda, Togo, Morocco, Madagascar, Sierra Leone, Burkina Faso, Nigeria, Kenya, Gabon, Benin, Angola na wenyeji Tanzania. Hizi ni nchi 26 kati ya nchi 49 zilizosaini na 48 zilizoridhia Mkataba huo kati ya nchi 55 wanachama wa Umoja wa Afrika. Pia, yapo baadhi ya mashirika ya kimataifa yaliyoshiriki kama vile Transparency International, Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), GiZ, na CIFAR.

Pamoja na nchi nyingine wanachama kutoshiriki maadhimisho haya ya pamoja, ni imani yetu kuwa ujumbe huu wa Rais Samia unazihusu pia na umezifikia. Sisi leo, kupitia safu hii, tunasema inawezekana Afrika isiwe mahali salama kwa walarushwa. Tumepanga mikakati mingi kupitia maadhimisho haya; tumebadilishana uzoefu wa jinsi ya kuzuia na kupambana na rushwa kwa mafanikio katika nchi zetu.

Juhudi hizo zikiwa za pamoja kama ilivyokuwa kwa maadhimisho haya ya pamoja, tutakuwa tunaongea lugha moja dhidi ya rushwa, nayo ni 'Afrika si ardhi ya kulea rushwa' ambayo itasambaa kupitia matendo yetu kama alivyoagiza Rais Samia. Tunaweza. Hakuna linaloshindikana kwa umoja wetu chini ya Umoja wa Afrika huku tukiunganishwa na utekelezaji wa dhati wa Mkataba wa Umoja wa Afrika wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa. Tunarudia, ***inawezekana kuifanya Afrika mahali pasipokuwa salama kwa walarushwa kwa vitendo vyetu dhidi ya rushwa. Aluta Continua. Mungu Ibariki Afrika. God bless Africa. Dieu bénisse l'Afrique.***

RAIS SAMIA: AFRIKA SI SALAMA KWA WALARUSHWA

- ☉Aagiza jengo la ofisi za AUABC kujengwa
- ☉Awataka Waafrika kutathmini nafasi zao katika mapambano dhidi ya rushwa
- ☉Asisitiza kuzingatia kaulimbiu ya kuzuia rushwa

Na Casiani Magogo, Arusha

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt, Samia Suluhu Hassan ametoa onyo kwa watu wanaojihusisha na vitendo vya rushwa ambapo amesema Afrika si sehemu salama kwa wala rushwa.

Rais Samia ametoa onyo hilo Julai 11, 2023 wakati wa kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika yaliyofanyika katika ukumbi wa Lake Nyasa uliopo Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC) kuanzia Julai 9, 2023.

Akiongea mbele ya wadau mbalimbali wa mapambano dhidi rushwa wa bara la Afrika, Rais Samia alisema moja ya vikwazo vikubwa vya maendeleo barani Afrika ni janga la rushwa. *“Walarushwa wafahamu kwamba nchi za Afrika si vichaka vya kuficha fedha zilizotokana na rushwa au kufuga wala rushwa. Tunataka dunia nzima ifahamu kuwa, Afrika si salama kwa walarushwa na hilo lionekane kwa kupitia vitendo vyetu* dhidi *ya rushwa”,* alisisitiza Rais Samia.

Pia, alitoa rai kwa wadau wote wa mapambano dhidi ya rushwa kutafakari na

kuchambua kwa dhati masuala ya rushwa ili kubainisha changamoto au vikwazo vya mapambano hayo na kuchukua hatua muafaka kuzitatua.

Katika hotuba yake, Rais Samia alieleza kuwa Serikali ya Tanzania iko mbioni kuhakikisha Ofisi za Bodi ya Ushauri wa Masuala ya Rushwa ya Umoja wa Afrika (AUABC) inakuwa na jengo lake la kudumu la kufanyia kazi zake jijini Arusha. *"Ninaielekeza Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa kushirikiana na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa kuhakikisha jengo hili linajengwa haraka",* alisisitiza Rais Samia.

Rais Samia aliwataka Waafrika wote wakiwemo Watanzania kutafakari na kutambua nafasi zao katika mapambano dhidi ya rushwa kwani rushwa inawanyima wananchi wa Afrika maendeleo kama huduma bora za afya, elimu au za maji safi na salama. Alisema rushwa pia inawanyang'anya haki waliyostahili wananchi fulani na kuwapa wale wasioistahili hivyo akamtaka kila mmoja kutumia vema nafasi zao kwenye mapambano dhidi ya rushwa ili kutokomeza rushwa barani Afrika.

Akirejea kaulimbiu ya TAKUKURU inayosema *'Kuzuia Rushwa ni Jukumu Lako na Langu,* Tutimize Wajibu Wetu', Mhe. Rais Samia alisema kaulimbiu hiyo inampa deni kila Mtanzania na Waafrika kwa ujumla kujipima endapo tunatimiza wajibu wetu katika mapambano dhidi ya rushwa na kuitokomeza katika jamii zetu.

Julai 11 ya kila mwaka ni siku maalum iliyotengwa na Umoja wa Afrika kuadhimisha Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika. Siku hii maaulum inatokana na maazimio ya Mkutano wa 29 wa Wakuu wa Nchi za Umoja wa Afrika uliofanyika Addis Ababa, Ethiopia Julai 3 – 4, 2017.

Maadhimisho ya mwaka 2023 kwa nchi wanachama wa Umoja wa Afrika yameadhimishwakwa ngazi ya bara nchini Tanzania katika jiji la Arusha.

Maadhimisho haya yalianza Julai 9, 2023 na kufikia kilele Julai 11, 2023 yakiambatana na kaulimbiu inayosema: *'Mafanikio baada ya Miaka 20 ya Utekelezaji wa Mkataba wa Umoja wa Afrika wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa na Matarajio Yake'*.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akisalimiana na Viongozi mbalimbali mara baada ya kuwasili AICC jijini Arusha wakati wa kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika Julai 11, 2023.

WADAU AFRIKA WASHIRIKI MATEMBEZI YA KUPINGA RUSHWA

Na Miriam Chisoro, Arusha

Wadau wa mapambano dhidi ya rushwa Afrika wameshiriki matembezi ya kupinga rushwa ikiwa ni sehemu ya ufunguzi wa maadhimisho ya Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa Barani Afrika mwaka 2023 yaliyofanyika kibara nchini Tanzania. Matembezi hayo yaliongozwa na Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mhe. Hemed Suleiman Abdullah akimwakilisha Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mhe. Hussein Ali Mwinyi.

"Leo tumeamka mapema kwa ajili ya kazi hii, kuunga mkono juhudi za Watanzania wote pamoja na viongozi

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar Mhe. Hemed Suleiman Abdulla akihutubia kufungua maadhimisho ya Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika jijini Arusha Julai 9, 2023

Bendi ya brass kutoka Shule ya Polisi Tanzania (CCP) ikiongoza matembezi ya kupinga rushwa yaliyokuwa sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika yaliyofanyika jijini Arusha, Tanzania Julai 9, 2023.

wetu katika mapambano dhidi ya rushwa na uhujumu uchumi," alisema Mhe. Hemed alipokuwa anahutubia kufungua maadhimisho hayo yaliyofanyika katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC) na kuhudhuriwa na mamia ya watu.

Shamrashamra za uzinduzi wa maadhimisho hayo zilianza mapema asubuhi ambapo wadau wa mapambano dhidi ya rushwa wa ndani na nje ya Tanzania wakiwemo wananchi wa Arusha walijitokeza kwa wingi katika eneo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Arusha. kwa ajili ya kushiriki matembezi ya kupinga rushwa.

Matembezi hayo yalianzia Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na kupita Mnara wa Saa ambapo ndiyo katikati ya bara la Afrika, kisha barabara ya Sokoine na kupita Mnara wa Mwenge wa Uhuru na kuishia viwanja vya AICC.

Wadau walioshiriki matembezi hayo ya takribani kilomita mbili ni pamoja na Wakuu wa Mamlaka za Kuzuia na Kupambana na Rushwa za nchi wanachama wa Umoja wa Afrika, wadau wa maendeleo, viongozi wa vyama vya siasa, watumishi wa Taasisi za Serikali wa sekta binafsi.

Pia, katika matembezi hayo walishiriki viongozi wa dini mbalimbali, wanafunzi, skauti, waandishi wa habari, wananchi wa Arusha, pamoja na viongozi na watumishi wa ZAECA na TAKUKURU.

Matembezi hayo yalipambwa na vikundi mbalimbali vya vijana wa hamasa, bendi ya Polisi pamoja na wanafunzi waliobeba mabango mbalimbali yenye ujumbe wa mapambano dhidi ya rushwa.

Baadhi ya mabango hayo yalibeba ujumbe *'KUZUIA RUSHWA NI JUKUMU LAKO NA LANGU', 'CORRUPTION SIO POA', 'PREVENT, DETECT, FIGHT CORRUPTION', na 'KUPAMBANA NA RUSHWA*

MHE. JOAQUIM: MAPAMBANO DHIDI YA RUSHWA YATAUNDA AFRIKA TUITAKAYO

Na Tezra Nkonya, Arusha

Makamu wa Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri wa Masuala ya Rushwa ya Umoja wa Afrika (AUABC), Mhe. Pascoal Antonio Joaquim amesema ni muhimu kila Mwafrika kushiriki mapambano dhidi ya rushwa ili kujenga na kuunda Afrika tunayoitaka.

Mhe. Joaquim alisema haya Julai 11, 2023 wakati akitoa salamu za Bodi hiyo katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika yaliyofanyika jijini Arusha, Tanzania.

Mhe. Joaquim alisisitiza kuwa kwa pamoja tunaweza kuzuia na kupambana na rushwa barani Afrika.

"Katika siku hii muhimu tunaangazia mapambano dhidi ya rushwa kama bara la Afrika. Miaka 20 iliyopita, siku kama ya leo Umoja wa Afrika ulichukua maamuzi haya muhimu ikiwa kama sehemu ya kuzuia na kupambana na rushwa", alisema Makamu huyo wa Mwenyekiti wa AUABC.

Mgeni rasmi katika kilele cha maadhimisho haya alikuwa

Makamu Mwenyekiti wa AUABC Mhe. Pascoal Antonio Joaquim akichangia mada wakati wa kongamano la Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika lililofanyika Julai 10, 2023.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akipokea tuzo kutoka kwa Makamu Mwenyekiti wa AUABC Mhe. Pascoal Antonio Joaquim wakati wa kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika Julai 11, 2023.

Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika huadhimishwa Julai 11 ya kila mwaka tangu mwaka 2017.

Maadhimisho ya mwaka 2023 yamekuwa ya kipekee kwa sababu imetimia miaka 20 tangu kusainiwa kwa Mkataba wa Umoja wa Afrika wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa wa mwaka 2003.

Mhe. Joaquim alisema Julai 11 ni siku muhimu sana kwa bara la Afrika kwani inatukumbusha hatua tuliyopiga katika mapambano dhidi ya rushwa yaliyoanza kwa umakini chini ya Mkataba wa Umoja wa Afrika wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa miaka 20 iliyopita.

"Ni muhimu kutambua mafanikio yetu katika mapambano dhidi ya rushwa ila pia ni muhimu kutambua changamoto tulizonazo na tunazopitia na kutafuta ufumbuzi wa kudumu," alisema Mhe. Joaquim.

"Inatia moyo kujua kuwa maendeleo kadha wa kadha na ajenda ndani ya Afrika zimeweka mkazo na kipaumbele katika mapambano dhidi ya rushwa na hii inatupa matumaini kwamba tutakabili na kulimaliza tatizo hili la rushwa," alisisitiza kiongozi huyo wa AUABC.

Mkataba wa Umoja wa Afrika wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa unatoa fursa ya ushirikiano na kubadilishana ujuzi baina ya nchi wanachama na kuona ni kwa namna gani bara la Afrika linaweza kuendeleza mapambano dhidi ya rushwa kwa mafanikio.

Nchi nyingi barani Afrika zimeharamisha rushwa na zina taasisi za kuzuia na kupambana na rushwa na zimeanzisha vitengo mbalimbali vinavyoshughulikia makosa ya rushwa ndani ya mamlaka za kisheria

SIMU: 113 *113# SMS 113
TAKUKURU APP
TAKUKURU TV
TAKUKURU.TZ takukuru.tz Takukuru Tz
PCCB

NI HESHIMA KWA TANZANIA KUWA MWENYEJI WA MAADHIMISHO YA SIKU YA MAPAMBANO DHIDI YA RUSHWA AFRIKA 2023

Na Eldora Liwa, Arusha

Waziri wa Nchi - Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene amesema Tanzania imepewa heshima kubwa kuwa mwenyeji wa maadhimisho ya Siku ya Mapambano dhidi ya Rushwa barani Afrika mwaka huu.

Mhe. Simbachawene aliyasema hayo Julai 11, 2023 wakati wa kilele cha maadhimisho hayo yaliyofanyika kuanzia Julai 9 – 11, 2023 katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC) jijini Arusha, Tanzania. Waziri huyo aliongea haya kabla ya kumkaribisha mgeni rasmi ambaye alikuwa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Pia alimshukuru Rais Samia kwa kukubali kuwa mgeni rasmi katika maadhimisho hayo. “Hii ni ishara ya utashi wako wa kisiasa wa kuzuia na kupambana na rushwa nchini Tanzania na barani Afrika kwa ujumla”, alisema Mhe. Simbachawene na akawashukuru wageni wote wa ndani na nje ya Tanzania walioshiriki maadhimisho hayo muhimu kwa maendeleo ya Afrika.

Akirejea historia ya maadhimisho hayo, Waziri Simbachawene alisema siku

hiyo huadhimishwa Julai 11 ya kila mwaka tangu mwaka 2017 ikiwa ni sehemu ya maazimio ya Mkutano Mkuu wa 29 wa Wakuu wa Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika uliokutana Julai 3 – 4, 2017 Addis Ababa, nchini Ethiopia.

Wakuu hao waliichagua siku hiyo kwa kurejea tukio muhimu la kihistoria la Julai 11, 2003 ambapo nchi wanachama wa Umoja wa Afrika zilisaini Mkataba wa Umoja wa Afrika wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa (African Union Convention on Preventing and Combating of Corruption – AUCPCC), jijini Maputo, nchini Msumbiji.

Waziri Simbachawene alimjulisha Rais Samia kuwa mwaka huu 2023, pamoja na kuadhimisha Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika, Umoja wa Afrika umeadhimisha miaka 20 ya utekelezaji wa Mkataba wa Umoja wa Afrika wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa.

Ni kwa sababu hii, kaulimbiu ya maadhimisho ya mwaka huu inasema ‘Mafanikio baada ya Miaka 20 ya Utekelezaji wa Mkataba wa Umoja wa Afrika wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa na Matarajio Yake’.

Mhe. Simbachawene pia alimjulisha Rais Samia kuwa katika siku tatu za maadhimisho hayo, wadau walishiriki matembezi ya kupinga rushwa, maonesho katika mabanda na kongamano la wadau lililojadili mada mbalimbali kuhusu mapambano dhidi ya rushwa barani Afrika.

Aidha, TAKUKURU, ZAECA na baadhi ya wadau wa maadhimisho hayo walishiriki mahojiano kupitia redio na televisheni kwa madhumuni ya kutoa elimu kwa umma.

Baadhi ya wadau wa mapambano dhidi ya rushwa wakimsikiliza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora Mhe. George Simbachawene (hayupo pichani) wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika jijini Arusha Julai 11, 2023

CP. HAMDUNI: TUMETUMIA MAADHIMISHO KUELIMISHA UMMA KUHUSU MAPAMBANO DHIDI YA RUSHWA

⊙ Zaidi ya wadau 700 washiriki maadhimisho

Eldora Liwa, Arusha

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) CP. Salum Rashid Hamduni amesema TAKUKURU imetumia maadhimisho ya Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika kuelimisha umma na kuuhamasisha ushiriki mapambano dhidi ya rushwa. Maadhimisho hayo yalihudhuriwa na zaidi ya wadau 700.

CP. Hamduni alisema hayo kwa nyakati tofauti Julai 9, 2023 na Julai 11, 2023 wakati akitoa maelezo ya utangulizi kuhusu maadhimisho hayo yaliyofanyika kibara jijini Arusha kuanzia Julai 9, 2023 hadi Julai 11, 2023. Alisema kupitia maadhimisho hayo, TAKUKURU na wadau wengine wameshiriki maonesho kwa siku tatu ambayo yalitumika kuelimisha umma kuhusu dhana ya rushwa, madhara yake na namna ya kuizuia na kupambana nayo.

Akitoa maelezo kuhusu maonesho hayo kwa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipotembelea banda la TAKUKURU katika viwanja vya AICC yalipofanyika maonesho hayo, CP. Hamduni alisema uelimishaji huo umefanyika kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa mapambano dhidi ya rushwa.

Wadau wengine walioshiriki maonesho hayo walikuwa Bodi ya Ushauri wa Masuala ya Rushwa ya Umoja wa Afrika (AUABC), Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi ya Zanzibar (ZAECA), Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma ya Zanzibar na Mamlaka ya Kudhibiti Madawa ya Kulevya (DCEA). Wengine ni Mamlaka ya Hifadhi za Taifa (TANAPA), Chama cha Skauti Tanzania (TSA), Tanzania Girl Guide Association (TGGA), na Anti – Corruption Voices Foundation (ACVF).

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akipata maelezo kutoka kwa Afisa kutoka Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) Insp. Johari Msirikale alipotembelea mabanda ya maonesho wakati wa kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika Julai 11, 2023.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akipata maelezo kutoka kwa Kamishna wa Uhifadhi wa TANAPA William Mwakilema alipotembelea mabanda ya maonesho wakati wa kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika Julai 11, 2023.

VIJANA WASHIRIKISHWE KATIKA MAPAMBANO DHIDI YA RUSHWA

Na. Sarah Chodota, Arusha

Vijana wanapaswa kushirikishwa katika mapambano dhidi ya rushwa kwa sababu ni mhimili mkubwa wa mabadiliko katika taifa lolote duniani ikiwamo kubadili mitazamo ya wanajamii ili kukabili tatizo la rushwa.

Kauli hii ilitolewa na Bw. Maxence Melo, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la JamiiForums wakati anawasilisha mada kuhusu *'Mchango wa Vijana katika Mapambano Dhidi ya Rushwa katika Ulimwengu wa Kidijitali: Matumaini baada ya Miaka Ishirini ya Utekelezaji wa Mkataba wa Umoja wa Afrika wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa'* katika kongamano la kuadhimisha Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika lililofanyika Julai 10, 2023 katika ukumbi wa Lake Nyasa katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha (AICC) kilichopo jijini Arusha, Tanzania.

Bw. Melo alisema pamoja na nafasi hiyo ya kuwa chachu ya mabadiliko, vijana wamekuwa miongoni wa waathirika wakubwa wa vitendo vya rushwa na ufisadi katika mataifa yao.

"Hali hii imesababisha vijana kukosa haki zao nyingi, nafasi zao katika eneo la utawala bora na uwajibikaji pia kuwafanya vijana waishi maisha ya kimaskini. Hivyo, kumshirikisha kijana na kumuwezesha kumesaidia taifa kusonga mbele", alisema Bw. Melo.

Akirejea takwimu za Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, alisema nchini Tanzania kundi la vijana ni kubwa Zaidi ikilinganishwa na wanajamii wengine.

"Watanzania wenye umri wa miaka sifuri hadi 34 ni asilimia 76 ya Watanzania milioni 62.5" na kufafanua kuwa takwimu hizi zinashahibiana na za maitafa mengine ya Afrika. Alieleza kuwa vijana hao barani Afrika wamekuwa wakipaza sauti zao kuhakikisha kuna kuwa na uwazi na uwajibikaji katika nchi zao.

Bw. Melo alisema kuwa asasi za kiraia nyingi zimetambua nafasi hii ya vijana katika jamii na zimewashirikisha vijana katika mambo mbalimbali ya kijamii. Alifafanua kuwa uzoefu huo unatoa fundisho kuwa mapambano dhidi ya rushwa hayatofanikiwa endapo vijana hawatoshirikishwa ili wawe sehemu ya safari yenyewe.

Akirejea uzoefu kuhusu matumizi ya mitandao ya kijamii, programu tumizi mbalimbali na teknolojia ya akili bandia, alisema vijana ndiyo watumiaji zaidi wa fursa hizi ambazo zimechangia kubadilisha mwenendo mzima wa mapambano dhidi ya rushwa kwa vijana.

"Fursa hizi zimetoa nafasi kwa vijana kujifunza, kutoa elimu, kuhoji na kutoa taarifa za vitendo vya rushwa" alisema Bw. Melo kuonesha jinsi gani ilivyo muhimu kwa mataifa kuendelea kushirikisha vijana katika mapambano dhidi ya rushwa.

Mada mbalimbali ziliwasilishwa katika kongamano hilo na kufuatiwa na mijadala iliyohusisha wadau wa mapambano dhidi ya rushwa wa ndani na nje ya Tanzania na bara la Afrika.

Kongamano hili lilikuwa sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika ambayo mwaka huu kwa mara ya kwanza imeadhimishwa katika ngazi ya bara nchini Tanzania.

Baadhi ya vijana ambao ni mabalozi wa mapambano dhidi ya rushwa wakiwa wamebeba mabango yenye ujumbe wa kuhamasisha mapambano dhidi ya rushwa tayari kushiriki matembezi ya kupinga rushwa ikiwa ni sehemu ya ufunguzi wa maadhimisho ya Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika jijini Arusha Julai 9, 2023

WADAU WAPONGEZWA KWA JUHUDI ZAO KATIKA MAPAMBANO DHIDI YA RUSHWA

Na Sarah Chodota, Arusha

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amepongeza juhudi za wadau kushirikiana na Serikali katika mapambano dhidi ya rushwa nchini.

Mhe. Rais Samia aliwataja wadau hao kuwa sekta binafsi, asasi za kiraia, taasisi za dini, vyombo vya habari na wadau wengine wanaoshiriki katika mapambano dhidi ya rushwa kupitia Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji (NACSAP).

Mhe. Dkt. Samia alisema haya Julai 11, 2023 jijini Arusha wakati akihutubia katika katika kilele cha maadhimisho Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika yaliyofanyika katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC).

Maadhimisho hayo yalihudhuriwa na wadau mbalimbali wa ndani na nje ya Tanzania wakiwemo Wakuu wa Mamlaka za Kuzuia na Kupambana na Rushwa za nchi wanachama wa Umoja wa Afrika.

Baadhi ya wadau walioshiriki maadhimisho hayo na kuhojiwa akiwamo Dkt. Ayub Rioba ambaye ni Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC) waliongelea nafasi na wajibu wao katika mapambano haya.

Akizungumzia nafasi ya vyombo vya habari katika

mapambano dhidi ya rushwa, Dkt. Rioba alisema vyombo hivyo vina fursa ya kushiriki mapambano haya kwa kuhabarisha umma kuhusu madhara ya rushwa katika jamii na kutoa vipindi vya redio au televisheni vya kuelimisha umma.

Alisema pia vina dhima ya kufanya habari za kiuchunguzi na kubainisha maeneo ambayo kuna rushwa ili Taasisi za Serikali au vyombo husika vichukue hatua,

Prof. Edward Hoseah
Aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu - TAKUKURU

Aliyewahi kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Prof. Edward Hoseah alishauri nchi za Afrika na dunia nzima kuamka kuzuia na kupambana na rushwa kwani kwenye rushwa hakuna maendeleo na wananchi wataendelea kupata shida rushwa ikiachwa ishamiri.

Naye Balozi Valentino Mlowola ambaye pia aliwahi kuwa Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU alisisitiza suala la wananchi kushiriki katika mapambano dhidi ya rushwa kwa kuwa madhara yake yanamgusa kila mtu kutokana na huduma za jamii kushindwa kupatikana kwa sababu za rushwa. Balozi Mlowola alisisitiza kuwa kila mtu anawajibika kupambana na rushwa.

Sheikh Mkuu wa Wilaya ya Arusha Hussein Said alizungumzia nafasi ya dini katika mapambano dhidi ya rushwa. Sheikh Said ambaye alisema viongozi wa dini kupitia maandiko matakatifu wanaweza kuhimiza waaumini wao kupinga vita rushwa. Alifafanua kuwa mtu anayemuogopa Mwenyezi

Sheikh Hussein Said
Sheikh Mkuu wa Wilaya - Arusha

Balozi Valentino Mlowola
Aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu - TAKUKURU

Mungu na ana hofu ya Mungu hawezi kuomba rushwa kwani kwa kufanya hivyo anakuwa amemchukiza Mwenyezi Mungu.

Naye Bw. Boyi Hamenyimana, mmoja wa vijana na mkazi wa Arusha aliyeshiriki maadhimisho alisisitiza vijana kuwa mstari wa mbele katika mapambano dhidi ya rushwa kwa kuwa rushwa imefanya vijana kukosa haki zao za msingi

Bw. Boyi Hamenyimana
Mkazi wa Arusha

RAIS SAMIA: MAPAMBANO DHIDI YA RUSHWA YAMEOKOA ZAIDI YA SHILINGI BILIONI 139

Na. Sarah Chodota, Arusha

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema juhudi mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali katika mapambano dhidi ya rushwa katika kipindi cha miaka mitatu zimefanikisha kuokoa zaidi ya Shilingi bilioni 139.

Akitaja baadhi ya mafanikio ya Tanzania katika mapambano hayo wakati akihutubia katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika Julai 11, 2023 jijini Arusha, Rais Samia alisema fedha hizo zilizookolewa na Serikali ni kiasi kikubwa cha fedha kwa umma ambazo angepewa fedha angezielekeza kuimarisha sekta ya afya nchini ili vituo na zahanati zilizojengwa ziwe na vifaa tiba.

“Fedha hizo ukinipa mimi sasa hivi nikifumba macho nakwambia nazipeleka kununua vifaa tiba”, alisema Mhe. Dkt Samia. Alisema pamoja na hatua hizo, bado zinahitajika jitihada zaidi kukabiliana na janga la rushwa kwa njia za uadilifu.

Rais Samia aliahidi kuwa Serikali itaendeleza juhudi za kuokoa fedha nyingi zaidi ili kunusuru fedha nyingi zisiende kwa wala rushwa bali ziende kuharakisha maendeleo ya wananchi.

Akielezea mafanikio mengine ya kukabili tatizo la rushwa ambayo ni sehemu ya utekelezaji wa Mkataba wa Umoja wa Afrika wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Mhe. Dkt. Samia alisema Serikali imeiimarisha TAKUKURU kwa kuipatia rasilimali fedha na rasilimali watu pamoja na kutunga na kuipitia Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ya mwaka 2007.

Alieleza kuwa Serikali imeanzisha na kuimarisha pia Taasisi za kusimamizi uwazi, uwajibikaji, haki na utawala bora. Hatua hizi zimeambatana na kutungwa kwa sheria mbalimbali ikiwamo Sheria ya Kuwalinda Watoa Taarifa na Mashahidi ya mwaka 2015.

Rais Samia alisema kuwa Serikali imeanzisha na kuimarisha utoaji wa huduma kwa umma kwa kutumia TEHAMA kwa huduma ambazo si lazima yawepo mawasiliano ya mtu na mtu ili kupunguza kuzungumza na kupatana hivyo kuzuia vitendo vya rushwa. Alizitaja baadhi ya huduma hizo kuwa michakato ya zabuni, usajili wa biashara, namba ya mlipa kodi na maombi ya kuunganishiwa umeme.

"*Pamoja na dosari za hapa na pale, tumefanya na tutaendelea kufanya vizuri zaidi katika matumizi ya fedha za umma na kuongeza uwazi na kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa*," aliahidi Rais Samia.

Picha ya vifaa tiba vilivyonunuliwa na Serikali kwa ajili ya moja ya hospitali zinazotoa huduma kwa umma.

ZAECA: TUNASHIRIKIANA NA WADAU KUZUIA RUSHWA

Na. Sarah Chodota, Arusha

Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi ya Zanzibar (ZAECA) inachukua hatua mbalimbali kwa kushirikiana na wadau kuzuia vitendo vya rushwa kabla havijajitokeza ndani ya Taasisi za Serikali na jamii.

Akitoa maelezo kuhusu utekelezaji wa kazi za ZAECA kwa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan alipotembelea banda la ZAECA katika maonesho ya maadhimisho ya Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika Julai 11, 2023, Mkurugenzi Mkuu wa ZAECA Bw. Ali Abdalla Ali alisema kati ya wadau hao ni Masheha ambao wameshirikiana kutoa elimu na kupata taarifa za vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi.

Bw. Ali alieleza kuwa ZAECA pia imekagua miradi inayotekelezwa na Serikali pamoja na kampuni na taasisi za nje ya nchi, imefuatilia matumizi ya fedha za Serikali katika utekelezaji wa miradi mbalimbali kama ya maji, elimu au ya afya.

Pia, Bw. Ali alisema ZAECA inawajibika pia kuzishauri Taasisi za umma kuhusu taratibu za kazi ili kuzuia vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi visitokee katika utoaji wa huduma.

Mkuu wa Mkoa wa Arusha Mhe. John Mongella (katikati) akiwa na wakuu wa Taasisi za Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU na ZAECA) na Mtendaji Mkuu wa Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha (AICC) Bw. Epharaim Mafuru (kulia) wakati wa kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika Julai 11, 2023.

Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama nchini, Jenerali Jacob John Mkunda akiwasili katika viwanja vya AICC jijini Arusha wakati wa kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika Julai 11, 2023.

Waliowahi kuwa Viongozi wa TAKUKURU kutoka kushoto Prof. Edward Hoseah, Bw. Ekwabi Mujungu, Mhe. Balozi (mst) CP. Valentino Mlowola na Meja Jenerali (mst) John Mbungo ni miongoni mwa wadau walioshiriki kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika Julai 11, 2023.

Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, Inspekta jenerali wa Polisi Camilius Wambura akiwasili katika viwanja vya AICC jijini Arusha wakati wa kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika Julai 11, 2023.

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar Mhe. Hemed Suleiman Abdulla akisalimiana na baadhi ya viongozi kabla ya kuongoza matembezi ya kupinga rushwa ikiwa ni sehemu ya ufunguzi wa maadhimisho Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika jijini Arusha Julai 9, 2023.

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar Mhe. Hemed Suleiman Abdulla akisalimiana na baadhi ya viongozi kabla ya kuongoza matembezi ya kupinga rushwa ikiwa ni sehemu ya ufunguzi wa maadhimisho ya Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika jijini Arusha Julai 9, 2023.

JARIDA
LA TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora Zanzibar Mhe. Haroun Ali Suleiman akizungumza kabla ya kuanza kwa matembezi ya kupinga rushwa. Kushoto kwake ni Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar Mhe. Hemed Suleiman Abdulla na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. George Simbachawene.

Baadhi ya Viongozi wa dini wakisubiri ufunguzi wa matembezi ya kupinga rushwa ikiwa ni sehemu ya ufunguzi wa maadhimisho ya Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika jijini Arusha Julai 9, 2023

Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU CP. Salum Hamduni na Naibu Mkurugenzi Mkuu Bibi Neema Mwakalyelye wakizungumza kabla ya kuanza kwa matembezi ya kupinga rushwa ikiwa ni sehemu ya ufunguzi wa maadhimisho ya Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika jijini Arusha Julai 9, 2023



Sheikh Hussein Said Ijunje akisoma dua kwa ajili ya matembezi ya kupinga rushwa ambayo yalikuwa sehemu ya ufunguzi wa maadhimisho ya Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika jijini Arusha Julai 9, 2023

Mkuu wa Mkoa wa Arusha Mhe. John Mongella akiwakaribisha wageni na wananchi kabla ya kuanza kwa matembezi ya kupinga rushwa ikiwa ni sehemu ya ufunguzi wa maadhimisho ya Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika jijini Arusha Julai 9, 2023

Mchungaji Dkt. Godson Abel Mollel akiombea matembezi ya kupinga rushwa ambayo yalikuwa sehemu ya ufunguzi wa maadhimisho ya Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika jijini Arusha Julai 9, 2023

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar Mhe. Hemed Suleiman Abdulla akiongoza matembezi ya kupinga rushwa ikiwa ni sehemu ya ufunguzi wa maadhimisho ya Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika jijini Arusha Julai 9, 2023. Pamoja naye ni baadhi ya Viongozi wa Serikali wa Tanzania na wa Mamlaka za Kuzuia na Kupambana na Rushwa.

Mkurugenzi Mkuu wa ZAECA Bw. Ali Abdalla Ali akitoa maelezo ya utangulizi wakati wa ufunguzi wa maadhimisho ya Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika jijini Arusha Julai 9, 2023.

Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU CP. Salum Rashidi Hamduni akitoa maelezo ya utangulizi wakati wa ufunguzi wa maadhimisho ya Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika jijini Arusha Julai 9, 2023

Wadau wa mapambano dhidi ya rushwa waliobeba mabango yenye ujumbe wa kuhamasisha mapambano dhidi ya rushwa wakati wa matembezi ya kupinga rushwa wakiwasili viwanja vya AICC jijini Arusha kwenye ufunguzi wa maadhimisho ya Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika jijini Arusha Julai 9, 2023.

Baadhi ya washiriki wakimsikiliza mgeni rasmi Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar Mhe. Hemed Suleiman Abdulla (hayupo pichani) wakati anafungua maadhimisho ya Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika katika ukumbi wa Lake Nyasa wa wa AICC jijini Arusha Julai 9, 2023.

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar Mhe. Hemed Suleiman Abdulla (kulia katika jukwaa) akipokea wadau wa mapambano dhidi ya rushwa waliobeba mabango yenye ujumbe wa kuhamasisha mapambano dhidi ya rushwa walioshiriki matembezi ya kupinga rushwa ikiwa ni sehemu ya ufunguzi wa maadhimisho ya Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika jijini Arusha Julai 9, 2023

Wadau wa mapambano dhidi ya rushwa wakionesha mabango yenye ujumbe wa kuhamasisha mapambano dhidi ya rushwa kabla ya kuanza ya matembezi ya kupinga rushwa ambayo yalikuwa sehemu ya ufunguzi wa maadhimisho ya Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika jijini Arusha Julai 9, 2023

Baadhi ya washiriki wakimsikiliza mgeni rasmi Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar Mhe. Hemed Suleiman Abdulla (hayupo pichani) wakati anafungua maadhimisho ya Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika katika ukumbi wa Lake Nyasa wa wa AICC jijini Arusha Julai 9, 2023.

Baadhi ya Wakurugenzi wa TAKUKURU wakifuatilia uwasilishaji wa mada wakati wa kongamano la maadhimisho ya Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika katika ukumbi wa Lake Nyasa wa AICC jijini Arusha Julai 10, 2023.

Mdau kutoka African Union Office of the Youth Envoy kutoka Nigeria Bw. Moses Uyang akichangia mada wakati wa kongamano la maadhimisho ya Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika katika ukumbi wa Lake Nyasa wa AICC jijini Arusha Julai 10, 2023

Makamu Mwenyekiti wa AUABC Mhe. Pascoal Antonio Joaquim akichangia mada wakati wa kongamano la maadhimisho ya Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika katika ukumbi wa Lake Nyasa wa AICC jijini Arusha Julai 10, 2023.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora Zanzibar Mhe. Haroun Ali Suleiman akihitimisha kongamano la maadhimisho ya Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika katika ukumbi wa Lake Nyasa wa AICC jijini Arusha Julai 10, 2023

Kwaya ya TAKUKURU ikitumbuiza na kuelimisha wakati wa ufunguzi wa maadhimisho Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika katika ukumbi wa Lake Nyasa wa AICC jijini Arusha Julai 9, 2023.

Kwaya ya TAKUKURU ikitumbuiza na kuelimisha wakati wa ufunguzi wa maadhimisho Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika katika ukumbi wa Lake Nyasa wa AICC jijini Arusha Julai 9, 2023.

Kwaya ya TAKUKURU ikitumbuiza na kuelimisha wakati wa ufunguzi wa maadhimisho Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika katika ukumbi wa Lake Nyasa wa AICC jijini Arusha Julai 9, 2023.

Kwaya ya TAKUKURU ikitumbuiza na kuelimisha wakati wa ufunguzi wa maadhimisho Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika katika ukumbi wa Lake Nyasa wa AICC jijini Arusha Julai 9, 2023.

Baadhi ya washiriki wakifuatilia majadiliano katika Kongamano la maadhimisho ya Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika katika ukumbi wa Lake Nyasa wa AICC jijini Arusha
Julai 10, 2023

Baadhi ya washiriki wakifuatilia majadiliano katika Kongamano la maadhimisho ya Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika katika ukumbi ukumbi wa Lake Nyasa wa AICC jijini Arusha
Julai 10, 2023.

Baadhi ya washiriki wakifuatilia majadiliano katika Kongamano la maadhimisho ya Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika katika ukumbi wa Lake Nyasa wa AICC jijini Arusha Julai 10, 2023

Baadhi ya washiriki wakifuatilia majadiliano katika kongamano la maadhimisho ya Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika katika ukumbi wa Lake Nyasa wa AICC jijini Arusha Julai 10, 2023.

Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU CP. Salum Hamduni (katikati) akiwa na Maafisa wa TAKUKURU Bi. Tulibako Minga (kushoto) na Bw. John Shija (kulia) katika banda la TAKUKURU kwenye maonesho ya maadhimisho ya Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika Julai 9, 2023.

Wadau wa mapambano dhidi ya rushwa wakitembelea banda la Anti - Corruption Voices Foundation (ACVF) kwenye maonesho ya maadhimisho ya Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika Julai 10, 2023.

Mkurugenzi Mkuu wa ZAECA Bw. Ali Abdalla Ali (kulia) akiwa na Maafisa wa ZAECA Bi. Saumu Ramadhan (katikati) na Bw. Yussuf Juma Suleiman (kushoto) katika banda la ZAECA kwenye maonesho ya maadhimisho ya Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika
Julai 9, 2023.

Vijana wa Skauti na Girl Guide wakiwa katika banda la Tanzania Scouts Association (TSA) kwenye maonesho ya maadhimisho ya Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika Julai 10, 2023.

Waziri wa Nchi - Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. George Simbachawene akihutubia kufungua kongamano la Maadhimisho ya Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika katika ukumbi wa Lake Nyasa wa AICC jijini Arusha Julai 10, 2023.

Mkurugenzi wa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) Dkt. Ayub Rioba akiongoza mjadala katika kongamano la Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika katika ukumbi wa Lake Nyasa wa AICC jijini Arusha Julai 10, 2023.

Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU CP. Salum Hamduni akitoa maelezo ya utangulizi kuhusu kongamano la Maadhimisho ya Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika katika ukumbi wa Lake Nyasa wa AICC jijini Arusha Julai 10, 2023

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu Dodoma Prof. Lughano Kusiluka akiwasilisha mada wakati wa Kongamano la Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika katika ukumbi wa Lake Nyasa wa AICC jijini Arusha Julai 10, 2023.

Wajumbe wa Kamati ya Maandalizi ya Maadhimisho ya Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika wanaojumuisha watumishi wa ZAECA na TAKUKURU wakiwa katika picha ya kumbukumbu mbele ya ukumbi wa Lake Nyasa wa AICC jijini Arusha Julai 10, 2023.

WAITIKIA WITO WA RAIS SAMIA: Baadhi ya washiriki wa maadhimisho ya Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika wakiwa katika lango kuu la kuingia Hifadhi ya Taifa ya Ngorongoro, mkoani Arusha Julai 13, 2023 kwa ajili ya utalii.

'ROYAL TOUR': Baadhi ya washiriki wa maadhimisho ya Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika wakipiga picha na wanajamii ya Kimaasai wanaoishi Hifadhi ya Taifa ya Ngorongoro, mkoani Arusha Julai 13, 2023.

UZURI WA TANZANIA HIFADHINI: Baadhi ya washiriki wa maadhimisho ya Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa barani Afrika wakimtazama tembo katika Hifadhi ya Taifa ya Ngorongoro, mkoani Arusha Julai 13, 2023.

JARIDA

LA TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

ISSN:0856 - 7670

TOLEO MAALUM

2023

TAKUKURU APP

TAKUKURU.TZ takukuru.tz Takukuru Tz

SIMU: 113 *113# SMS 113

Jarida hili hutolewa na Kurugenzi ya Elimu kwa Umma ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU)
Mtaa wa Jamhuri S.L.P 1291,
41101 DODOMA, Tanzania.
Simu: (026) 2323316, Nukushi: (026) 2323332,
Baruapepe: dgeneral@pccb.go.tz
Tovuti:www.pccb.go.tz

KUZUIA RUSHWA NI JUKUMU LAKO NA LANGU; TUTIMIZE WAJIBU WETU